



Ofisa Mkuu wa Tigo Pesa, Angelica Pasha, akitambulisha promosheni mpya ya wiki ilitwayo "Pesa Mwaa Mwji na Tigo pesa" jijini Dar es Salaam jana, ambayo itawawezesha wateja wa Tigo Pesa kuondoka na zawadi za fedha taslimu hadi Sh. milioni 325. Kushoto ni Meneja wa Wateja Maalumu wa Tigo Pesa, Mary Rutta. **PICHA:**

MPIGAPICHA WETU

Nyamanga alisema miradi hii ni nyenzo mojawapo ya kupunguza na iwapo itawezekana kuondosha kabisa matumizi ya zebaki katika shughuli za uchimbaji mdogo wa dhahabu kwa kuhamasisha matumizi ya teknolojia mbadala ili kulinda afya ya binadamu na mazingira kwa ujumla.

Wasiochanja mifugo yao waonywa Bariadi

Na Happy Severine, BARIADI

KAIMU Ofisa Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi, Magdalena Gwandu, amesema wananchi wasiojitokeza kwa hiari kuchanja mifugo yao watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria zinazoongoza Sekta ya Mifugo.

Gwandu alisema hayo jana wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika kwenye Ukumbi wa Bariadi Motel mjini Bariadi.

Alisema wananchi ni lazima

watambue kuwa kuchanja mifugo chanjo za magonjwa mbalimbali ni lazima na si hiari na atakayekiuka atachukuliwa hatua za kisheria.

Kaimu Ofisa Mifugo huyo alisema kwa kipindi cha miezi sita (Oktoba hadi Machi) wamechanja mifugo 300 kati ya mifugo 8000 iliyopo ndani ya halmashauri hiyo, idadi ambayo ni kidogo.

Alisema uchanjaji wa mifugo haukufikia lengo walilojiwekea la kuchanja nusu ya mifugo yote iliyokuwapo kutokana na

mwitikio mdogo wa wananchi ambao wamekuwa wagumu na wabishi kupeleka mifugo yao kuchanjwa.

Aliongeza kuwa tayari wameshatoa elimu juu ya umuhimu wa chanjo kwa mifugo na wanaendelea kutoa elimu ili wachanje idadi kubwa ya mifugo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi, Elias Masanja, alilagiza idara ya mifugo kuenyelea kutoa elimu ya chanjo ili wananchi wengi wajitokeze kuchanja mifugo yao.

Alisema mbali na chanjo za mbuzi, ng'ombe, kondoo na kuku, pia waendeleo kutoa chanjo kwa mbwa na kuwaua wale wanaozagaa mitaani.

Baadhi ya madiwani walisema kumekuwa na kero ya mbwa wengi wanaozagaa ovyo mitaani na kusababisha madhara kwa binadamu, hasa watoto wadogo.

Walisema mbwa wengi walioko mitaani hawajachanjwa na pindi wanapong'ata binadamu wanasababisha madhara makubwa na kutomba

serikali kupitia idara hiyo kughibiti tatizo hilo kwa kuwaua mbwa wote 'wasioeleweka mitaani'.

"Ni vyema zoezi la uchanjaji mbwa liwe endelevu ili kuweka kinga kwa wananchi wetu wanaoathirika kupitia mbwa na pia wafanye msako wa kuwaua mbwa wote wa mitaani," Robert Rweyo, Diwani wa Somanda, alisema.

Juma Musa, mkazi wa Bariadi, alishauri elimu zaidi itolewe ili wananchi wajue faida za kuchanja mifugo yao.